
# Ee Sayuni Umtukuze

(Sekwensia ya Ekaristi Takatifu)

Na. Joseph Makoye
Handcopy: F.B. Mallya
Recopied: Sinkonde Lameck






2. Shangilio la rohoni lipendeze liwe zuri sifa tele livume
Ipo leo siku kubwa kwa kumbusho la kuwekwa kwanza ile karamu
//Muda ule umekwisha ipo meza ya mfalme na sheria ya sasa
Tumepata mapya yote nuru siyo nusu giza mwanga siyo usiku x2

3. Tendo lake karamuni Kristo ametuamuru tutende tumkumbuke
Twafuata amri yake tukitoa hii sadaka kwa mkate na divai
//Mkate wageuka mwili na divai yawa damu kanuni kwa wakristo
Huelewi huioni kweli hiyo ukubali kwani ni mwujiza mkuu x2

4. Unaona tu maumbo ni alama zifumbazo utukufu wenyewe
Ule mwili unywe damu kila umbo linamfumba Yesu mzima halisi
Ukipewa tu kimego umempata Yesu mzima si yake tu sehemu
Mmoja hula elfu hula wote hupokea sawa na mpokewa hakomix2

5. Hula wema na wabaya kwa bahati mbalimbali kifo au uzima
Basi mkate mtakatifu huwa sumu kwa wabaya dawa bora kwa wema
//Ikimegwa sakramenti usisite uamini Yesu yu ndani yake
Mwili wake haumegwi ni alama ivunjwayo hali yake ni sawa x2

6. Ee mkate wa malaika huwalisha wasafiri si mkate wa kafiri
Hii mifano ya zamani kutolewa mwana isaka na kondoo kuchinjwa
//Ee mchungaji wetu mwema Yesu utuhurumie tuchunge utulinde
Ee mchungaji wetu mwema tuonyeshe mema yako huko kwenye wazima x2

7. Ee mchungaji wetu mwema Ee mwenyezi na mjuaji utuchunge na sisi.
Tujalie pia huko kushiriki meza yako na raia mbinguni
//Ee mchungaji wetu mwema ee mwenyezi na mjuaji utuchunge tulinde
Tujalie pia huko kushiriki meza yako na raia mbinguni x2